

desnaji Meja io yao
ya umeme kuharakisha katika usambazaji wa ukuaji wa maendeleo kwa wananchi.

UTURU UK 18.

Bilioni 4.5/- kuboresha vituo atamizi vya ufugaji

Misungwi
NA BALTAZAR MASHAKA

SERIKALI imetenga sh. bilioni 4.5 zitakazotumika kuboresha vituo atamizi na mifugo kwa lengo la kuwawezesha vijana kujijiri. Pia, imekabidhi madume bora 36 ya ng'ombe aina ya boran kwa Halmashauri ya Buchosa wilayani Sengerema mkoani Mwanza, ambayo yatagawiwa kwa vikundi vya wafugaji ili kuboresha mifugo ya asili.

Akizungumza katika halifa ya kukabidhi madume hayo juzi kwa Mkuu wa Wilaya ya Sengerema, Senyi Nganga, Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, alisema Serikali ya Awamu ya Sita inafanya jitihada kuwatoa vijana katika umasikini kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Alieleza katika kutimiza azma hiyo, Wizara ya Mifugo imetenga sh. bilioni 4.5 zitakazotumika kuboresha mifugo na kutoa mafunzo ya kwa vijana.

Ulega alisema vijana 70 tayari wameanza mafunzo ya biashara, ufugaji wa tija, ujenzi wa mabanda, kuandaa mashamba ya malisho, namna ya kupata mifugo inayofaa kunenepeshwa na mafunzo kwa vitendo kupitia programu maalumu Atamizi ya Samia kwa Ufugaji wa tija ambapo baada ya kuhitimu watakabidhiwa ng'ombe 10 kila mmoja.

"Programu hii inalenga kuboresha mifugo ya asili ambapo zimetengwa sh. bilioni 3.5 za kuboresha mashamba ya mifugo nchi nzima, kati ya hizo sh. milioni 866 zimetumika kununua mitamba 873 na madume bora 366, lengo mifugo iliyopo iwe na tija," alisema.

Naibu waziri huyo alisema madume hayo yatagawiwa kwa vikundi vya wafugaji ili kuboresha mifugo ya asili na kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na mchango wa pato la Taifa kupitia sekta ya mifugo kwa kuzalisha maziwa na nyama nyingi kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje.

Ulega aliziagiza halmashauri zote nchini kuwamilikisha ardhi wafugaji kwa mujibu wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025, Ibara ya 40 (1) inayoelekeza kupima ardhi na kuwamilisha wafugaji.

Naye, mkuu wa wilaya hiyo, Nganga alisema changamoto kubwa ya wafugaji ni ufugaji wenye tija kwani wanachokipata hakilingani na nguvu wanayotumia kwa sababu ya kutofuata kanuni za ufugaji bora.

"Vijana mliopata fursa msiliangushe serikali, kupata madume bora tija itaongezeka hivyo mtumie elimu na mtaji mtakopata kuongeza vipato. Ng'ombe hao sio wa majaribio ni kodi ya Watanzania, tunataka mkazalishe kwa vitendo," alisema mkuu huyo wa Wilaya ya Sengerema.

Mmoja wa wafugaji kutoka Buchosa, Eliasi Kapel, alisema madume hayo yatawasaidia kupata mbegu bora ya ng'ombe wa nyama na maziwa kwani ukuaji wake ni wa haraka ukilinganisha na ng'ombe wengine wa asili.